karibuni.

"Si hivyo tu, lakini Serikali ya Manispaa

tili wa kingono, ambayo ni muhimu katika kushughulikia visa hivyo.

NIPASHE UK 9

*

# Wazee kimila wafugaji wakutana kujadili mgogoro ulishaji mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** LONGIDO

ATHARI za mabadiliko ya tabianchi na usimamizi wa nyanda za malisho katika Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, umewakutanisha pamoja viongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai na serikali, kwa ajili ya kujadili utatuzi wa migogoro na hasara inayotokana na changamoto hizo.

Mkutano huo, ulioitishwa na Shirika la Watu na Wanyamapori Tanzania (TPW), linalotekeleza mradi wa ardhi kwa maisha, uliongozwa na Ofisa Mazingira kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Theodori Mlokosi.

Mkurugenzi wa TPW, Neovitus Sianga, alisema majadiliano hayo yanahusu njia bora za kusimamia nyanda za malisho na kushughulikia changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Sianga, alisema kikao hicho pia kilijadili pamoja na mambo mengine, uwekaji wa mikakati madhubuti itakayowezesha jamii za eneo hilo, kuepukana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Kikao kilijikita pia kujadili maandalizi ya mipango ya msimu ujao wa malisho, ikizingatia mwanzo wa mvua katika eneo hilo.

...Tunataka kuanzisha mikakati ya kuimarisha usimamizi wa malisho, kwa kuzingatia hali ya hewa na rasilimali zinazopatikana kwenye maeneo haya," alisema Sianga.

Mmoja wa viongozi wa mila, Saroni Kayogo, alisema wako tayari kutoa mchango wao wa kiasili na utamaduni.

"Sisi viongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimasai, tunalishukuru sana Shirika la TPW, kwa elimu na mafunzo waliotupa ya usimamizi wa nyanda za malisho na namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa ajili ya kuokoa mifugo kipindi cha kiangazi," alisema Kayogo.

Ofisa wa Mazingira wa TAMISEMI, Theodori Mlokosi, alisema matokeo ya kikao hicho ni hatua kubwa kuelekea kujenga ushirikiano imara, kati ya serikali, mashirika ya kiraia na jamii za asili.

"Kwa ujumla, kikao hicho kilimalizika kwa matumaini makubwa kwa mustakabali wa usimamizi wa malisho na mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi katika eneo la Longido na maeneo mengine yanayofanana nchini Tanzania.

"Kila mshiriki aliondoka akiwa na azma imara ya kuchukua hatua na kutekeleza mikakati iliyokubaliwa ili kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na ustawi wa jamii."

CamScanner

# Wazalishaji, wauzaji vyakula mifugo wasiofuata taratibu kushughulikiwa

Na Mwandishi Wetu

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi kupitia Wakala ya Maabara ya Veterinari nchini (TVLA), imetangaza kuwashughulikia wazalishaji na wauzaji wa vyakula vya mifugo wasiofuata sheria na kanuni zinazoongoza utekelezaji wa shughuli hizo.

Mtendaji Mkuu wa Wakala hiyo, Dk. Stella Bitanyi, alisema hayo mwishoni mwa wiki, alipokuwa akitoa taarifa fupi ya yaliyobainika wakati wa operesheni maalum iliyoendeshwa na timu ya wataalam kutoka ofisini kwake kwa kushirikiana na wakaguzi wa vyakula vya mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambao walifanya ukaguzi katika viwanda vinavyozalisha na maduka yanayouza vyakula hivyo katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, kuanzia Novemba 30 hadi Desemba mosi, 2023.

Dk. Bitanyi aliwataka wazalishaji wote wa vyakula vya mifugo nchini kuzalisha vyenye uwiano sahihi wa viinilishe vinavyohitajika kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa na mamlaka ya kuthibitisha ubora wa vyakula hivyo (TBS) na vya kimataifa kwa wale watakaohitaji kusafirisha nje ya nchi.

"Tunawaagiza kila kundi la chakula wanalozalisha wahakikishe sampuli yake inapelekwa kwenye maabara kuu ya veterinari ambao ndio wenye ithibati ya kitaifa ya kuchambua vyakula vya mifugo ili waweze kuthibitisha na kutoa vyeti vya ubora," alisema Dk. Bitanyi.

Aidha, aliwataka wazalishaji kupima malighafi zote wanazotumia kutengeneza vyakula vya mifugo na kuwaelekeza kusajili taasisi na mahali wanapozalishia vyakula hivyo.

"Tunafahamu kwamba usajili ni kila mwaka, ambao hawajasajiliwa wafanye hivyo na wale ambao tayari wameshasajiliwa waendelee kuhuisha usajili wao kupitia tovuti ya wizara ambako watapata maelekezo yote ya kufanya mazoezi hayo," alisema Dk. Bitanyi.

Akitoa malekezo upande wa wauzaji wa vyakula hivyo, Dk. Bitanyi aliwataka kununua vyakula vyao kutoka kwa wazalishaji waliothibitishwa kwenye viwango vya ubora kwa kila kundi la chakula wanalotaka kununua kwa wazalishaji hao.

Akizungumza na timu ya wataalam hao mmoja wa wazalishaji wa vyakula vya mifugo kutoka mkoani Pwani, Samson Maro, ameipongeza serikali kwa kufanya zoezi hilo mara kwa mara na kuahidi kuyafanyia kazi aliyoshauriwa na wataalam hao.

Mmoja wa wauzaji wa chanjo na vyakula vya kuku na bata kutoka mkoani humo, Domitila Melisa, amewaeleza wataalam hao namna anavyowasaidia wafugaji kwenye eneo lake kuwapa elimu na ushauri kuhusu aina ya chakula wanachopaswa kupewa ndege hao kulingana na umri walionao.

Akizungumzia hali yake ya ufugaji kabla ya kupewa elimu inayohusu vyakula vya mifugo, mfugaji wa kuku kutoka Kibaha, mkoani Pwani, Mwajuma Mwami, alisema alikuwa akinunua vifaranga na chakula cha kuku kwa kubahatisha jambo lililokuwa linasababisha vifo vya mara kwa mara vya vifaranga hao na kuiomba serikali kufanya ukaguzi na uhakiki wa viwanda na maduka ya vyakula vya mifugo kuwa endelevu.

Uzalishaji wa vyakula vya mifugo nchini unasimamiwa na Sheria ya Nyanda za malisho na chakula cha mifugo ya mwaka 2010 pamoja na kanuni zake zilizoandaliwa mwaka 2013, kwa pamoja vinawataka wazalishaji na wauzaji wa vyakula hivyo kuhakikisha wanyama wanapata vyakula bora ili waweze kuongeza uzalishaji wa mazao yao.